

HALMASHAURI YA WILAYA YANGARA
TAARIFA FUPI KITENGO CHA CHANJO HADI JUNI 2018

UTANGULIZI

Wilaya ya Ngara ina jumla ya vituo 53 vinavyotoa huduma za chanjo kati ya vituo 61 vilivyopo katika wilaya kwa mwaka 2018. Vituo visivyotoa chanjo ni 7 ambavyo 3 ni vya binafsi na 4 ni majeshi, 1 ni kipya cha serikali. Kwa mwaka 2018 wilaya ilipewa walengwa 16,821 ambao ni watoto chini ya mwaka mmoja (surviving infants), walengwa kwa mwezi ni watoto 1,402. Na idadi ya wakazi wote 391,181.

MAFANIKIO

- Kuanzia mwezi Januari hadi Juni mwaka huu 2018 uchanjaji ulifanyika kwa kiwango cha watoto 7896 sawa na 94% kwa chanjo ya Penta1, na watoto 7690 sawa na 91% kwa Penta3.
- Pia chanjo dhidi ya Surua/Rubella tumechanja watoto 7614 kwa Surua Rubella1 =91%, na watoto 6432=79% kwa Surua Rubella2.
- Pamoja na kuwa na kiwango hicho bado tuna watoto 206 ambao au hawakupata chanjo au waliasi chanjo na mikakati ya kuwatafuta inafanyika kwa kutumia wenyeviti wa vitongoji na wahudumu wa Afya wa vijiji katika maeneo yao.
- Kwa mwezi wilaya inatakiwa kuchanjawatoto 1,401 hivyo kwa miezi sita tulitakiwa kuchanja watoto 8406 lakini tumechanja watoto 7690 ambayo ni sawa na 91% kwachanjo ya Penta dozi ya 3, lakini pamoja na kuchanja bado tuna watoto 206 walioasi na kutokamilisha chanjo na hii ni tofauti kati ya Penta ya 1 na Penta ya 3.

NB:

Hii ni kutokana na baadhi ya changamoto ambazo zingine ziko nje ya uwezo wetu katika kuzitatua.

CHANGAMOTO

- Baadhi ya frige ni mbovu na hakuna spea zake.
- Upungufu wa chanjo dhidi ya polio tangu mwezi Juni 2018
- Uchache wa watumishi vituoni/ugeni kwa baadhi ya watumishi waliopewa usimamizi wa shughuli za chanjo kwa kutokuwa wamepewa mafunzo kabla,

MAPENDEKEZO

- Tunaomba wizara ifanye mchakato wa kutuongezea majokofu kwani vituo vimeongezeka kutoka 48 mwaka 2014 hadi 53 mwaka 2018
- Upatikanaji wa chanjo ya kukinga ugonjwa wa kupooza wizara ilianganalie kwa karibu suala hili.
- Kuendeleakutoa huduma za chanjo kila siku katika vituo vyote vinavyotoa huduma za chanjokila siku,
- Uhakiki wa taarifa ngazi ya wilaya, hii inafanyika kila wakati wa kuwasilisha taarifa kwa kuleta vitabu vyote na kuzifanyia uhakiki pamoja na mtumishi mhusika akiwepo.